

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA ARUSHA:**

Anwani ya simu "REGCOM"

Simu Na. 2545608/2502289/2545870

Fax Na: 2545239 / 2544386

Barua Pepe: [rasarusaha@yahoo.com](mailto:rasarusaha@yahoo.com)

Barua Pepe: [ras.arusha@pmoralg.go.tz](mailto:ras.arusha@pmoralg.go.tz)

Website: [www.arusha.go.tz](http://www.arusha.go.tz)

Unapojibu tafadhali taja:



**OFISI YA MKUU WA MKOA,  
S.L.P. 3050,  
ARUSHA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.**

Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Mrisho Mashaka Gambo ametoa msaada wa Bati arobaini (40) kwa Mzee Michael Mwita Askari (Veterani) aliyeshiriki Vita ya Pili ya Dunia.

Akikabidhi msaada huo wa Bati 40 kutoka kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa pamoja na Shilingi laki tatu (300,000/=) za Kitanzania zilizotolewa na Ofisi ya Mshauri wa Jeshi la Akiba Mkoa wa Arusha, Katibu Tawala Mkoa wa Arusha Bw. Richard Kwitega amemtaka Mzee Mwita (Veterani) kutumia msaada huo wa Bati 40 kwa ajili ya kujenzi wa nyumba yake ambayo iliungua kwa moto hivi karibuni.

Bw. Kwitega amesema msaada huo ni ahadi ya Mhe. Mkuu wa Mkoa kumsaidia Mzee Mwita mara baada ya kupata taarifa kuwa nyumba yake aliyokuwa akiishi imeungua kwa moto na kwa sasa amekuwa akihifadhiwa na majirani pamoja na familia yake.

"Mhe. Mkuu wa Mkoa ameguswa sana na janga lililokupata la kuunguliwa nyumba yako kwa moto na kwa sasa hauna mahali pa kuishi na hivyo amenituma nikukabidhi msaada wa Bati 40 na pia pokea hizi Tshs 300,000/= ikiwa ni msaada toka Ofisi ya Mshauri wa Jeshi la Akiba Mkoa wa Arusha ili ziweze kukusaidia katika ujenzi", alisema Bw. Kwitega.

Mzee Michael Mwita ambaye alizaliwa tarehe 26/06/1923 kwa sasa ana umri wa miaka 96 na alishiriki Vita Kuu ya Pili ya Dunia huko Ethiopia (Abyssinia) ameishukuru sana Serikali kwa kumpatia msaada huo wa Bati 40 na Shilingi laki tatu ambazo zitamsaidia kuanza ujenzi wa makazi yake upya kwenye Kitongoji cha Eso-Unga Limited Arusha.

Naye, Mshauri wa Jeshi la Akiba Mkoa wa Arusha, Luteni Kanali Ally Haniu amesema Jeshi linakumbuka Mchango wa wapiganaji wake hivyo walivyosikia tukio waliguswa kuchangia Shilingi laki tatu kwa lengo la kumstili Mzee Michael Mwita (Veterani).

Imewasilishwa na;  
Kitengo cha Habari na Mawasiliano,  
Mkoa wa Arusha.

**28 APRIL, 2020**